# UZURI WA UMOJA

*Zaburi 133.*

Na - Nicholas kioko
23/03/2026




1. Palipo mapendo na Mungu yupo pale, (yupo pale) anatufundisha tupendane siku zote.

2. Mapendo ya kweli yatoka kwake Mungu, (kwake Mungu) wenye kupendana Mungu anaishi nao.

3. Anatufundisha tuishi ki-ndugu, (ki-ndugu) tusiwe na wivu tusiwe na chuki kamwe.

4. Tusiwe wagomvi tusiwe wafitini, (wafitini) pasipo na mapendo Mungu hapapendi.

5. Kumpenda jirani ndio kumpenda Mungu, (penda Mungu) anatufundisha tupendane siku zote.

6. Mapendo ya kweli sio ya siku moja, (siku moja) mapendo ya kweli ni ya siku zote milele.

All Rights Reserved